




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA



23/10/2024.

## TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya **shilingi milioni miambili kumi na saba na themanini na tisa elfu (217,089,000/=)** zimetengwa katika mwaka 2024/2025. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za serikali za mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

**Vikundi vinavyopaswa kuleta maombi vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:**

- I. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri.
- II. Kikundi kinachojishughulisha na shughuli za ujasiliamali mdogo au wakati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiliamali,
- III. Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano(5) na kuendelea na kikundi cha watu wnye ulemavu kiwe na wakikundi wasiopungua wawili (2) . pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu Mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zinafanana na za vikundi vingine.
- IV. Kikundi kiwe na akaunti benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiliamali na
- V. Wanakikundi ni lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kieletroniki (tembelea tovuti; [mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz](http://mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz)) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na afisa maendeleo ya jamii wa kata husika au mtendaji wa kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na vitambulisho vifuatavyo; Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji, Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **12/11/2024**

Tangazo hili limetolewa na:

  
Khalid A. Khalif

**Mkurugenzi Mtendaji.**

